Maelezo kwa Ajili ya Amani

Sura ya 9

Somo la Kusikiza: Agano Jipya #63

Shabaha: Kuelewa masharti ya amani ya Mungu.

Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. Hatimaye ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo.

- Wafilipi 4:6-8

Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini.

- Isaya 26:3

Katika Wafili 4, Paulo alipeana mashauri ya kutumika – maelezo yake kwa maisha ya Ukristo – yaliyolenga amani. Paulo alikuwa akiongea juu ya amani ya Mungu, hali ya amani ambayo Mungu anaweza kutuweka ndani yake ikiwa tunakutana na masharti ambayo ameweka. Paulo alielezea masharti kumi na mbili ndiyo sisi tupate amani ya Mungu maishani mwetu.

Kwanza ni kutosumbuka kwa ajili ya jambo lolote. Hata kama Paulo alikuwa gerezani, bado angetuhimiza tusisumbuke. Pili ni kuomba juu ya kila jambo. Tatu ni tafakari juu ya mambo mazuri. Ongoza mawazo yako badala ya kuyaacha yakutawale. Nne, Paulo aliwatia moyo Wafilipi wafanye mambo ambayo wamejifunza kutoka kwake. Alisema wafanye yale wanajua na kuamini kuwa ni sawa.

Sharti la tano kwa amani ya Mungu lilikuwa ni kutoswali thamana ya mazuri ambayo umefanya. Kazi zetu nzuri huwenda zisizawadiwe katika maisha haya lakini huko mbinguni. Sita kuwa mwenye shukrani. Paulo alikuwa na chaguo la kuhuzunikia yale ambayo hakuwa nayo au kumshukuru Mungu kwa yale aliyokuwa nayo, kama vile ushirika wake na Kristo. Tuna chaguo hilo pia. Saba ni kuwa wapole. Kukubali hali zetu kama mapenzi ya Mungu badala ya kupigana nayo huleta amani. Sharti la nane la amani ya Mungu ni kuwa na subira. Tunapaswa kujifunza kumngojea Bwana. Tisa, kumbuka ukaribu wa Bwana wako. Bwana kila mara husimama pamoja nasi, hata kama watu wengine wanatuacha. Kumi, pata furaha yako kwa kumjua Kristo na kukua kwa ukaribu naye. Kumi na moja, thamini kuthibitishwa na Mungu, juu zaidi ya kuthibitishwa na

watu wengine. Kumi na mbili, weka mioyo yenu na nia zenu ndani ya Kristo, ukijua kuwa anaweza kufanya kle aimbacho wewe huwezi kufanya.

1. Ukweli au uongo? Yesu alikuja kuleta amani ya dunia pamoja na wokovu.

2. Ukweli au uongo? Katika Luka 2, Yesu alipozaliwa, malaika waliahidi amani kwa watu wote.

3. Ukweli au uongo? Amani ya Mungu inawataka waumini kufanya mambo kadhaa.

4. Ukweli au uongo? Isaya 26:3 inaahidi amani ya Mungu kwa watu wote.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

5. Kwa nini unafikiria Paulo aliandika kuwa hatupaswi kusumbuka? *(Chagua yote yanaolingana)*
    a. Kusumbuka kunatoa mtazamo wetu kwa Mungu
    b. Kusumbuka kunatuibia amani ya Mungu
    c. Kusumbuka kunaweza kubadilisha hali zetu
    d. Yesu alitwambia tusisumbuke

6. Kwa nini tunapaswa kuomba badala ya kusumbuka? *(Chagua yote yanayolingana)*
    a. Mungu alituamuru kuomba
    b. Kuomba kunaweza kutukumbusha kuwa Mungu yuko uskani
    c. Tunaweza mwomba Mungu neema ya kupitia hayo na kumtukuza katika hali zetu
    d. Yote yaliyotajwa hapo juu.

7. Kwa nini kuwa mtu wa shukrani ni kitu cha muhimu sana? *(Chagua yote yanayolingana)*
    a. Inatupea nafasi ya kuringia watu wengine
    b. Inatusaidia kutoa mawazo kwa mambo ya kinyume na kuyaweka kwa mambo mazuri
    c. Inatukumbusha juu ya uaminfu wa Mungu kwetu
    d. Inatukumbusha juu ya yale tusionayo

8. Baadhi ya mambo gani unayoweza kushukuru Mungu juu yake hata katika hali ngumu? *(Chagua yote yaliyosahihi)*

a. Upendo wa Mungu na kipawa cha wokovu
b. Baraka na uaminifu wa Mungu
c. Ahadi ya kwamba Mungu hatawahi kutuacha
d. Yote yaliyotajwa hapo juu.

9. Ni vipi mawazo yetu yanaweza kutusaidia tupate amani ya Mungu? *(Chagua yote yaliyosawa)*

a. Tunaweza kuwaza juu ya mambo mazuri.
b. Tunaweza kuwaza juu ya Yesu
c. Tunaweza kukumbuka uaminifu wa Mungu kwetu wa nyakati zilizopita
d. Tunaweza kuyaweka juu ya jinsi tunavyoweza kubadilisha hali zetu

10. Kila mara huwa tunajaribiwa kufanya kilichorahisi badala ya kilichosahihi. Kwa nini kufanya kilichosahihi huleta amani? *(Chagua yote yaliyosahihi)*

a. Kufanya kilichorahisi kila mara hufanya maisha kuwa bora
b. Kufanya kilichosahihi hutuvuta karibu na Mungu
c. Kufanya kilichosahihi husaidia kujenga imani yetu tunavyomtumainia kutulinda.
d. Kufanya kilichosahihi humtukuza Mungu

Soma tena Wafilipi 4:6-8. Andika chini mambo ambayo yanakusumbua. Ombea kila moja ya mambo hayo sasa, na uulize amani ya Mungu ijaze maisha yako. Mwombe akusamehe kwa kutomtumaini na kwa kusumbuka. Muulize aweke nia yako ikimwelekea yeye na akusaidie kumtumaini. (Isaya 26:3) _____
_____
_____

Kwa nini tufurahi katika Bwana? Kwa nini furaha yetu ije kwanza kwa kumjua tu Kristo? Furaha yako inategemea nini? _____
_____
_____

Mshukuru Mungu kwa kipawa cha amani. Muulize akusamehe kwa kusumbuka. Muulize akusaidie kuweka mawazo yako juu yake na akusaidie kumtumaini. (Isaya 26:3) Mshukuru kwa yale yote ambayo amekupa. Muulize akusaidie uweke katika matumizi masharti haya ya mani.

KUZAMA ZAIDI

1. Kwa sababu hii “amani ya Mungu” ni hali ambayo Mungu anaweza kutuweka ndani mfululizo na ni ya masharti, tunawezaje kutumia kila moja ya masharti kumi na mawili ya amani, ambayo yanaweza kuitwa “Maelezo ya kupata amani” yaliyofundishwa na Paulo katika sura hii kuu?

_____
_____
_____

2. Elezea ni gani kati ya masharti haya ambayo ni ngumu kwako kutunza. _____
_____
_____
_____

3. Katika njia iyo hiyo, gani kati ya masharti haya lililokuletea mapito ya matunda ya amani ya Mungu, ulipotimiza sharti hilo? _____
_____
_____

4. Itakuwaje kama ungekariri masharti haya 12 na kisha kuomba kupitia ndani yake kila usiku kabla ya kulala? _____
_____
_____

5. Elezea jinsi unavyofikiria kwamba kutafakari mambo mazuri 8 ambayo Paulo anataja (katika aya 8) kutachangia hali yako ya binafsi ya amani ya Mungu. _____
_____
_____
_____

6. Unaweza kuhusisha vipi ujuzi huu kwa amani ya Mungu inayoelezewa na Nabii Isaya katika Isaya 26:3? _____
_____
_____

7. Nakupa changamoto la kukariri na kuishi na masharti haya 12 kwa mwezi mmoja na uone kile yanachangia kwa ujuzi wako wa binafsi wa hali ya amani inayoelezewa kama “amani ya Mungu.” Ni kwa njia kama gani unayodhani maisha yako yatabadilika kama matokeo ya kufanya hivyo? _____
_____